TANGAZO LA SERIKALI NA. 222 la tarehe 28/3/2025

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA USHURU WA MASOKO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME YA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 415 la 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2025, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ushuru wa Masoko ya Halmashauri ya Wilaya ya Same ya Mwaka 2024 ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya kanuni ya 3

2. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 3 katika tafsiri ya msamiati "afisa mwidhiniwa" kwa kuingiza maneno "na Mkurugenzi" katikati ya maneno "aliyeteuliwa" na "kusimamia".

Kufutwa kwa kanuni ya 11

3. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 11.

Marekebisho ya kanuni ya 16

4. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 16 kwa kuongeza mara baada ya kanuni ndogo ya (4) kanuni ndogo mpya ifuatayo:

> "(5) Kwa madhumuni ya kanuni hii, "kanuni za afya" maana yake ni miongozo au taratibu zinazowekwa ili kuhakikisha afya bora kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla.".

Marekebisho ya kanuni ya 23

5. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 23 kwa kufuta maneno "atakuwa ametenda kosa ana akipatikana" na badala yake kuweka maneno "anayetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii, akipatikana".

Marekebisho ya kanuni ya 24

6. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa kwa kufuta kanuni ya 24 na kuiandika upya kama ifuatavyo:

"Kufifilisha kosa

24. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kulipa ushuru anaodaiwa.".

Dodoma,
10 Januri, 2025

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi-OR-TAMISEMI*